

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



29 Agosti, 2019

TAARIFA KWA UMMA

ZUIO LA MATUMIZI YA MIFUKO LAINI YA PLASTIKI

Wananchi katika Jiji la Dar es Salaam wamezuiliwa kutumia Mifuko ya Plastiki kuanzia tarehe 01 Juni, 2019 kwa mujibu wa Kanuni za “Marufuku ya Matumizi ya Mifuko ya Plastiki za mwaka 2019” zilizoandaliwa chini ya Sheria za Mazingira ya Mwaka 2004. Pamoja na kuwa wananchi wengi wameacha kutumia mifuko hiyo, bado wengine wanaendelea kutumia **Mifuko Laini ya Plastiki** kama vifungashio vya biadhaa mbalimbali.

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam inawaelekeza wananchi, wafanyabiashara na wazalishaji wa **Mifuko Laini ya Plastiki** kuacha kuizalisha, kuiuza, kuisambaza na kuitumia mifuko hiyo. Kwa atakayekiuka zuio hilo adhabu ya faini au kifungo gerezani itatolewa kwa mujibu wa sheria. Ni vema kuendelea kutunza mazingira kwa manufaa ya wananchi wote na **kutii Sheria bila Shuruti**.

Sipora J. Liana

**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM**